

SwahiliWeb

ELECTRONIC DEPOSITORY AND RESOURCE ARCHIVE

www.swahiliweb.net

Archive: Pat Caplan

Document: Conversation with Salum Nassor

File reference: SW/PC/13034

This document has been downloaded from the SwahiliWeb archive on the understanding that it is copyright under the laws of the United Kingdom and the Berne Convention, and that no further copying, storage or distribution, in any form or by any means, including electronically, is permitted except under the provisions of fair dealing.

Copyright of all materials deposited with SwahiliWeb remains with the copyright holder. Those seeking copyright and associated permissions will be referred to the copyright holder.

Conversation with Salum Nassor, Kanga village, Mafia Island.

Taped 2002 by Pat Caplan. Transcribed by Joseph Bwaithondi, 2010

Salum Nassor was my neighbour and one of my greatest friends in Kanga village. He was also my most faithful correspondent over many years until his death in his eighties. His wife Masuda was also a good friend and informant, and so was one of their daughters Mgeni, who died in her forties. I also knew well most of the other ten children in this family. The idea of this meeting in 2002 when he was eighty years old was to record his life history but unfortunately most of the life history section did not record and what remains is a conversation about a variety of local current matters

Side A of tape

SN: Mimi nimezaliwa katika kijiji cha Bweni, Mafia mwaka 1922.

(big gap unrecorded – this was his life history)

PC: Ujana wako ukitazama hali ya kijiji hiki na ukitazama hali yake siku hizi unaona mabadiliko gani?

SN: Mabadiliko zamani mfano wake ni kuwa hawajuhi mambo ya tamaa wala habari za uridadiridadi lakini sasa kuna mabadiliko watu wanajua, wanaelewa mfano habari nydingi wanazipata sawa sawa ambazo zamani zilikuwa hazipatikani za nje. Mambo ya majonzi majonzi haya, matumizi ya mambo haya. Sasa naona hali wakati huu imekunjuka imekuwa ni nzuri kidogo. Na kama wamesisimka na watu wamekuwa binadam kamili.

PC: Ndio sawa

SN: Sasa wanajua jema na baya mtu na wanapofanya ni kwa kukusudia tu kama hivi mambo ya magonjwa ya dizaini hii zamani hakuna. Zamani hapa hapa nafahamu hospitali ipo Mafia tu moja na dokta alikuwa bwana Sabuni ambaye niliwhi kumuona mimi. Ukienda hospital utawakuta labda watu watatu wamelazwa pale pale mjini hamna watu. Sasa ukienda hospitali Kilindoni watu vitanda havikuenea hamna na hospitali utaona ni safi zamani walikuwa wanalamika haisafishwi. Zamani ilikuwa hakuna, utaweza kuona vitambaa vya vidonda vimetupwa. Sasa kidogo uangalifu hupo.

PC: Na siku zile za nyuma watu walikuwa wanacheza ngoma kama Kitanga na Mkobero nk?

SN: Walikuwa wanacheza sana tena sana tu ndio ilikuwa ni kazi yao hasa baadhi ya kusini/kaskazini. Walikuwa wanapenda sana kucheza vitanga na ndio kama mfano waganga wao wameamini sana ilikuwa.

PC: Ndio maana kule umewahi kuona ngoma,

SN: Ngoma hakuna ,ngoma zao ni za mchezo. Hakuna ngoma za kishetani.

PC: Niliwikia kwamba waganga wamekuja hapa Mafia kutoa uchawi.

SN: Mimi mambo haya hayaniingi sana lakini ndio nimesikia kutoa uchawi na bado wapo Bweni. Wanatoa uchawi na hapa nasikia kama wataitwa,lakini akili yangu inaona hii ni kama ah!

PC: Wanasema leo kwamba wanaweza kutoa chupa mwilini mwako, na wengine wameona sijuhi mkono wa mtoto mchanga.

SN: Nimesikia hayo mama, lakini mimi sioni ajabu maanake unajua kuna hawa wasaki/ waindi wanafanya kila mchezo wanaweza kumeza kamba unamuona sasa vipi. Muindi anaweza kukuambia wewe ushaokota mayai inuka hapo. Na ukiinuka unao mayai chini. Si ujanja tu?

PC: Kabisa

SN: Mimi sikubali naona upuuzi tu.

PC: Wanatisha watu tu. Kama wanaingia katika nyumba yako wanasema chupa hiki.

SN: Haya fukua hapa wanatoa kitu. Pengine kuna waonywa. Sasa watakutia aibu na hayo si kweli. Sasa utakataa mimi sijuhi sikufanya haya mambo.si kweli hapana bwana.

PC: Lakini hapo watu wanaogopa wanga.

SN: Watu wanapaogopa sana. Sasa hivi juzi juzi wanga sijui walikuwa wanatoka wapi wakaanguka na ungo Tanga. Hakusikia?? Yupo mwanga mmoja ameanguka na Ungo Tanga. Alikuwa anatoka kumsindikiza mtu pemba wakati wa kurudi mafuta yameisha, wakampeleka hospitali. Hospitali hakukaa muda akapona, alipotoka akakanyagwa na gari. Sasa kwa nini hakukanyagwa siku si zake ni maneno tu .

PC: Kicheko

SN: Wanasema wanatembea na ungo usiku ni wanga wana ndege wana basi, wanatembea huku. Inawezekana

PC: Labda

SN: Lakini mimi umri wangu miaka 80 na zama za ujana wangu natoka hapa kufata gari Kirongwe usiku.

Side B of tape

SN: Anashindwa kufyeka huyu

PC: Kweli

PC: Sasa itakuwaje na hii inataka nini sera za serikali au vipi?

SN: Serikali serikali.

PC: Kama nini??

SN: Serikali yaani imearibu hali ya uchumi wote. Watu wa chini hawana pesa. Unapeleka nazi zinakaa sokoni pengine siku mbili bila kuuza. Zamani nazi zinapiganiwa kwa foleni.

PC: Mh!

SN: Na hakuna mtu hasie pesa mfukoni mwake. Ilikuwa kama siujaliwa pesa vile wanafanya biashara pesa zinakuja na kutoka, manake wanafanya biashara. Soko linazunguka linakwenda. Unachouza kinanunuliwa mara moja.

PC: Mh!

SN: Sasa hivi hakuna .

PC: Sasa itakuaje hapa Kanga watakapo jenga mahotelii mawili pale Pwani?

SN: Sijui mimi naona labda wao wanategemea hao wageni tu. Sio imejengwa kwa kwa watu wa hapa.

PC: Ah! Kwa watalii tu.

SN: Watalii tu ndio. Sasa labda watatuleta pesa kidogo, pesa ya watalii itakuja na vile vile kutakuwa na watumishi na watumishi ni watu wa hapa. Na sasa zile pesa itasambaa zitatoka katika mikono ya watalii, zitakwenda kwa mmiliki wa hoteli, mmiliki wa hoteli atatoa vibarua na atawlipa msharaha watu/watumishi wake na wao watakuja kununu vitu kama vile kuku kwetu mayai nini na tutakuwa tunaneemeka kidogo.

PC: Labda sijui. Sasa sijuhi wengine wanaogopa watazuiliwa wasitumie Pwani.

SN: Eh Pwani sasa hivi nimesikia jangwa ile wamezuia.

PC: Nasikia wamesimamisha kwa muda

SN: Kwa muda

PC: Sijui kama watendelea baadae au vipi, unaonaje mpango huu?

SN: Mpango huu kuchukua jangwa lile sawa na kula sumu

PC: Mh!

SN: Kwasababu hii ni njia kubwa ya kwenda Kirongwe

PC: Ndio,

SN: Wale watu wote Wajimbo pale ndio bandari ya kuitisha bidhaa zao mashua zinaingia kuchukua nazi pale, sidhani kama watapata ruhusa kwenda Punda pale watajenga seng'enge. Na kwa sisi tuotaka kwenda Kirongwe kama hauna gari inabidi uende kwa miguu kwa njia ya Balale.

PC: Ni njia ndefu sana.

SN: Ni ndefu sana na ni maili 11 kutoka Kirongwe, hii hapa ni maili 8. Ingawa mji utachamka watapata pesa. Lakini pesa zake ngumu kidogo eh. Kwa mfano hii bandari kuu ya Rasini nazi zote tunapakia pale

PC: Mh!

SN: Mali yetu kutoka Dar salaam tunapakulia pale,sasa wakija wale hawataki ghasia.

PC: Ndio

SN: Wanakuja wageni wao wanataka faraga na salama. Sio karaha tu manake mswahili .kwa mtu mweupe hamwamini.

PC: Eh hii ndio tabu moja lakini wale wanaotaka kujenga pale ni wahindi,

SN: Wahindi hawa .

PC: Ndio wale wale wa Tanzasca SN: Ah!

PC: Baada basi sijuhi itakuaje manake watu wa Jimbo hawataki hata kidogo

SN: Watu wa Jimbo hawataki hata kidogo. Na hapa walikataa kwanza kidogo lakini baadhi ya wengine wahitaji wakakubali na wengine hawakukubali tena wakaungana wote.

PC: Hawakukubali wote.

SN: Hawakukubali wote. Hata huko msikitini wengine hawakukubali wote. Wengine mapaka leo hawajachukua pesa tunaambiwa bado zipo benki.

PC: Ndio

PC: Basi tutatazama mbele.

SN: itakavokua kama tutakua hai bado na sie tumeshakwisha tena basi wataona watoto wetu

PC: Ndio

SN: Kama itakuwa neema wataona wao au karma basi wataona wao. Sie tumeshakwisha tena.

PC: Mh!

SN: Hii si ya leo wala kesho itachukua muda.

PC : Ndio

SN: itachukua muda.

PC: Hatuwezi kujua mara moja.

SN: Itachukua muda. Na la tangu kupima hapa kiwanja na kuweka mawe kule sasa leo karibia imeshapita mwaka na zaidi . Wala kuwaona hawawaoni hapa hawajaja.

PC: Sasa mimi sijuhi itakuwaje na sio maeneo mawili tu maana nasikia wanataka kununua Bweni na wamenunua maeneo mengine kule Mtende.

SN: Kule Mtende wameshamaliza nasikia weshanunua maeneo mengi sana, na huku kwa yule Kinazi kule alipokuwa anakaa Yasini Kimanzi kule Bweni

PC: Mh!

SN: Wakawahi kuleta magodoro nasikia wakati wa krimasi na Mahema lakini halafu wakakatazia ,

PC: Wakakataziwa na nani?

SN: Serikali. Kwasababu wanasema yeye alipitia kule na huku kijiji hakijuhi. Sasa kijiji kinakupeleka kule ulipoacha urudie kule kule na sasa hivi hapa hajaja. Sasa sijuhi tena. Lakini yule mikondo yake ameacha yeye . ilikuwa aanzie kijijini huku mpaka, kama amengepata hawa hamnazo wameuza wenyewe hawa, si serikali ingesahihisha tu. Lakini hawa baada ya kule kuelekezwa serikali wao wakaja wanataka kuanza kujenga. Wakaleta ghasia zao za magodoro na nini ikawa tena watu wakashtuka. Basi kuulizwa tu bwana huku hukupitia basi hauwezi kupata

PC: Kiutaratibu.

SN: Kiutaratibu.

PC: Ndio

SN: Lakini mama watapata tu fedha watapata tu .

PC: Sisi kwa kiingereza tunasema fedha ina maneno mengi.

SN: Ndio Fedha ina maneno mengi inasema. (*hana anasema maneno ya Kiarabu magumu*) hakika fedha inamzika mke na mume haiba ya ukali ya huzuni/huzuri hata Pub/ baa fedha imetuika vizuri tu ya kisure .

PC: Ndio

SN: Hii ni kwa ajili ya fedha tu.

PC: Lakini wengine baadae wanasketika manake fedha wanatumia mara moja halafu baadae watakula nini.

SN: Hawana kitu ndio kama hivi nasikia Masha aliuza kule Bweni alichukua fedha katika kikapu akafungua Mahoteli akanunua maboti lakini leo hamna. Shamba sehemu ambayo inayomuogopa mie ndio bado nipo. Na pale kama atakuja Tajiri kutaka shamba lile basi mimi sina nguvu. Mie pale sikahi. Na ndio maneno mtaani nitaambiwa kwamba wewe umadhuri wako katika umma ni madogo kabisa. Lakini hawa wanaokuja watatia umadhuri katika umma mkubwa kabisa kwa hivyo wewe hatukuendekezi.

PC: Ndio

SN: Chukua kama utachukua kama hautaki basi. Mimi nikimiliki shamba kwa hati yangu hawawezi kupindua mkataba.,

PC: Ndio ni kweli mh!

PC: Sasa wanasema watakuja kupima lini?

SN: Hivyo walivyoniambia kuwa wanatengeza vibao vile manake hawana vibao vingine, vile vile vibao wanatengeneza na kweli wamethibisha watakuja.

PC: Sawa

SN Mh!

PC: Sawa.

SN: Mh Na mkurugenzi kanimbia kuwa nitawapa saruji, Mahingika akaitwa (ofisa wa Elimu) ili atupatie mifuko miwili ya saruji lakini tukapinga tunataka msaada wa watu wawili wa kuvyatua matofali yale. Mmoja Maharufu mmoja Salehe na kama hawana watamuhanjiri mtu huku.

PC: Haya tutazama kama watakuja sijuhi.

SN: Watakuja tena hawa nikawaambia tena zaidi nikamwambia kwa Mahingika Faraga tazamaa msione uzito kama kuna neno zaidi mnataka nyie mpata tunaweza kusaidieni tukajuanana, sio hivyo sivyo.

PC: Lakini wakati umenua shamba hilo mbona hakupimwa?.

SN: Niliponunu shamba hili alikupimwa lakini naona kama linalipiwa /limelipiwa kama Rent

PC: Ah! Sawa

SN: shilingi 20 kwa mwaka.

Kicheko wote

SN: Sasa nilivyopata mimi shamba kununua ile hati hasa akumalizika nilipata Argument

PC: Sawa

SN: Hat, shamba nimenunuai ni shilingi 4500

PC: Ah!

SN: Wakili kuandika hati anataka kiwango cha shilingi 1000 sasa nikapata Argument tu. Sasa ili shamba katika mwaka 65 bwana Athumanu alikuwa anadai dawa hii yake migomba ni yake. Kwa bahati nikapewa Argument na nikapewa na Cheti photocopy Nairobi wakaniletea mie. Ile Rent ya lease ndio akanisidia kufukuza Uchoyo. Uchoyo unamjua mwalimu Athumanu yule

PC: Ah!

SN: Maneno mengi. Uwezi kukaa hapa ameshalipia hati shilingi 20. mie nimeacha tena sikulipa Sasa nataka nimiliki kabisaaa.

PC: Sawa haya mimi naona tumezungumza sana .Na wewe labda